BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA NA MASHIRIKA YA UMMA (LAAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA 2017/2018 NA 2019/2020

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyenzi Mungu Azza wa Jalla kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu na muhimu ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma (LAAC) uliolenga kwenye Ripoti mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama zifuatazo;

1. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na
2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Sambamba na kuzingatia matakwa ya Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, Toleo la mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukurani za dhati kwa Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali kwa mashikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, tunatoa shukurani za pekee kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kuipatia mafunzo Kamati hii ili iweze

kutekeleza shughuli zake kwa wepesi na kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Katibu wa Baraza pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza hilo kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha katika muda wote ambao Kamati hii ilipokuwa ikiwajibika.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya LAAC, Makatibu Kamati pamoja na Maafisa kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa umahiri wao wa hali ya juu waliouonesha hadi tunawasilisha Ripoti hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo:

1. Mhe. Habib Ali Mohamed - Mwenyekiti;
2. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Makamo Mwenyekiti;
3. Mhe. Bakar Hamad Bakar - Mjumbe;
4. Mhe. Haji Shaaban Wazir - Mjumbe;
5. Mhe. Mwaanasha Khamis Juma - Mjumbe;
6. Mhe. Shaib Hassan Kaduara - Mjumbe;
7. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe;
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu;
9. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu;
10. Ndg. Hamad Akida Hamad - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti;
11. Ndg. Mwajuma Hassan Iddi - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti; na
12. Ndg. Juma Mohammed Juma - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti.

2.0 YALIOBAINIKA KWA KILA RIPOTI

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, Kamati ya LAAC ilizifanyia kazi Ripoti mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za miaka miwili tofauti pamoja na kuzingatia maelekezo ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2020. Katika kutekeleza shughuli hiyo, Kamati hii iliyafanyia kazi maeneo matatu kama ifuatavyo:

1. Mapato na Matumizi ya Serikali za Mitaa na Taasisi Zinazojitegemea za Umma;

2. Ukiukwaji wa taratibu mbali mbali zilizofanywa na Serikali za Mitaa na Taasisi Zinazojitegemea za Umma; na

3. Hali ya Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za Umma.

Mheshimiwa Spika, katika kuyafanyia kazi maeneo hayo baadhi ya mambo yafuatayo kwa ujumla wake yamebainika na maelezo kamili kuhusiana na yaliyobainika ni kama inavyoonekana kwenye Ripoti kuu ya Kamati hii ambayo inapatikana kwenye "tablet"

zenu.

1. Taarifa za Mapato na Matumizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi - Toleo la 2020, Kamati ya LAAC ina mamlaka ya kuchunguza hesabu za mwaka za mapato kwa zile Taasisi zinazokusanya mapato pamoja na kuchunguza matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma Zinazojitegemea kwa kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa kufanya uchunguzi kwa njia yoyote ile ambayo Kamati hii itaona inafaa juu ya mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali na Asasi zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imehisi ni vyema ikalisema suala hili kwa kuwa asilimia kubwa ya Taasisi za Serikali zilikuwa zina ugumu wa kutoa mashirikiano kwa Kamati hii pale inapohoji taarifa za mapato, matumizi ya kazi za kawaida na matumizi ya kazi za maendeleo na hata hudiriki kuieleza Kamati kuwa wao hawana hoja kwa hiyo hawaoni mantiki ya Kamati kufika katika Taasisi zao.

Mheshimiwa Spika, mtazamo huo wa Watendaji hubadilika baada ya Kamati kufika katika Taasisi zao na kuibua mambo mbali mbali muhimu waliyokuwa ama hawayajui au wameyatekeleza kimakosa bila ya wao kubaini kasoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri wa kuutoa hapa ni pale Kamati yako ilipofika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) ilipoieleza Kamati hii kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 imeokoa na kurejesha kiasi cha Tsh. 275,717,302 kupitia makosa mbali mbali, kama vile, matumizi mabaya ya mali na mapato, matumizi mabaya ya ofisi na kusafirisha magendo, isipokuwa kwamba, fedha hizo wanazoziokoa huwa haziripotiwi na Mamlaka kama ni mapato na wala hazioneshwi kwenye Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) ya Mamlaka, jambo ambalo ni kwenda kinyume na taratibu za kihesabu kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo huwekwa tu kwenye akaunti ya hesabu ambayo imefunguliwa tarehe 07 June, 2019 na hadi kufikia tarehe 15 Septemba, 2021 akaunti hiyo ina jumla ya Tsh. 146,268.739.71.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imeona hiyo ni kasoro kubwa na ilimuomba Mtendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa maelezo juu ya fedha hizo na hasa ikizingatiwa kuwa Taasisi yao imefanya ukaguzi katika Ofisi hiyo na haikuweza kubaini jambo hilo muhimu kwa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matakwa hayo ya Kamati, Mtendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliieleza Kamati kuwa, kasoro hiyo imejitokeza

ama Mkaguzi husika hakuwa na uelewa juu ya fedha hizo zilizookolewa pia Watendaji wa Mamlaka hawakumueleza au kutokana na ufinyu wa muda, Mkaguzi huyo hakuweza kupata muda mzuri wa kufanya majadiliano na Watendaji wa Mamlaka. Hata hivyo, aliieleza Kamati kuwa fedha hizo zinatakiwa kuoneshwa kwenye Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka ya Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka hii kuziingiza fedha wanazozikusanya kwenye Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka na fedha hizo wazitambue kama ni mapato halisi ya Mamlaka. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mamlaka haina uwezo kisheria wa kuzitumia fedha hizo basi mapato hayo yasomeke kuwa ni Taarifa ya Hesabu ya Amana "Deposit Account" na endapo fedha hizo zitawasilishwa Hazina basi fedha hizo zisomeke kuwa ni "Transfer".

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuandaa utaratibu mzuri utakaoielekeza Mamlaka kuhusiana na matumizi bora ya fedha wanazozikusanya kwa maslahi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kwa upande wa matumizi Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 800,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo, hata hivyo, hadi mwaka wa fedha 2019/2020 unamalizika fedha hizo hazikuingizwa. Kutokuingizwa kwa fedha za kazi ya maendeleo kumeifanya Mamlaka kutozitolea taarifa fedha hizo kwenye Taarifa yake ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC ilimtaka Mhasibu wa Mamlaka kuieleza Kamati kwa nini hakuijumuisha taarifa hiyo kwenye Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka na aliieleza Kamati kuwa alikuwa hajui kama inapaswa kuingizwa kwa kuwa haikuingiziwa fedha na alizidi kuieleza Kamati kuwa alivyoulizia suala hilo Wizara ya Fedha na Mipango alielekezwa kuwa taarifa hiyo asiingize kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni kasoro kubwa kihesabu na hasa ikizingatiwa kuwa tayari Baraza la Wawakilishi liliidhinishia Mamlaka hii kiasi hicho cha fedha kwa matumizi hayo. Hivyo, kitendo cha kutokuoneshwa shughuli hiyo kuwa haikuingiziwa fedha na Serikali kisichukuliwe kama ni kigezo cha kutoijumuisha taarifa hiyo kwenye Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka.

Mheshimiwa Spika, athari kubwa inayopatikana endapo taarifa hiyo haikujumuisha kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ni kutokujulikana kama shughuli

husika ilipangiwa fedha katika mwaka husika na fedha hizo hazikuingizwa kama ilivyotarajiwa. Kitendo hicho kinaweza kuitia nguvu Serikali na kuweze kuiingizia fedha shughuli hiyo katika mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati ya LAAC iliitaka Mamlaka kuhakikisha kuwa inaingiza kwenye Taarifa yake ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka taarifa zote za fedha ilizokadiriwa kutumiwa ili iweze kujulikana ni kiasi gani cha fedha ambacho hakikupatikana katika mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasoro hizo zilizobainika na Kamati yako juu ya Taasisi hii, Watendaji wa Mamlaka walikiri mbele ya Kamati hii kuwa licha ya kuwa Baraza kazi yake ni kuisimamia Serikali lakini pia hutoa mafunzo juu ya utendaji wa Taasisi kwa kupitia Kamati za Baraza. Hivyo, Kamati ya LAAC inawaasa Watendaji wote wa Umma kuzipa mashirikiano ya dhati Kamati hizo kwa maslahi ya taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, licha ya ugumu ilioupata Kamati hii kwa baadhi ya Taasisi wakati wa kufuatilia hoja ya mapato yaliyokusanywa na Taasisi husika, hata hivyo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Kitengo cha Mapato kinazipangia Taasisi kukusanya mapato ambayo hayana uhalisia, jambo linalopelekea kuonekana Taasisi hizo kuwa hazikuwajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuthibitisha kauli yangu hiyo naomba kulitolea mfano Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) ambalo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kukusanya Tsh. 1,500,000,000.00 katika vianzio vyake vya ndani na lilifanikiwa kukusanya jumla ya Tsh. 793,735,630.94 sawa na asilimia 52.9 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilitaka kujua sababu zilizopelekea Shirika hilo kushindwa kukusanya mapato hayo kama lilivyokadiriwa na liliieleza Kamati kuwa makadirio hayo ni makubwa na waliieleza Taasisi husika juu ya jambo hilo, hata hivyo, walitakiwa kukusanya kiwango hicho. Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, Kamati ilitaka kujua wastani wa mapato ambayo Shirika hilo linaweza kukusanya na ilielezwa kuwa lilipendekeza kunakohusika kukusanya jumla ya Tsh. 800,000,000 ambazo linahisi ndio uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya Taasisi zinaviacha vianzio vyengine vya mapato ambavyo wanauhakika kuwa vitakusanya fedha katika mwaka husika na endapo mapato yatapatikana basi mapato hayo huingizwa kwenye kifungu cha mapato mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imekitia mashaka kitendo hiki na imezitaka Taasisi kuweka makadirio kwa vile vianzio vya mapato ambavyo wanauhakika navyo kuvipata.

Mfano, mapato yanayotokana na kuuzwa kwa nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya Taasisi bado haivitumii ipasavyo vianzio vyao vya mapato jambo linalopelekea Taasisi hizo kutoa mchango mdogo kwa Serikali. Kwa mfano, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe Zanzibar inamiliki nyumba eneo la Mazizini hata hivyo, sehemu ya nyumba hizo wanaishi watendaji wa Mamlaka bure pamoja na kuwa wanalipwa mshahara kama kawaida na sehemu zilizosalia za nyumba hizo zinakodishwa.

Vile vile, kwa mujibu wa kifungu cha 42 cha Sheria ya Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe namba 4 ya mwaka 2010 Mamlaka hii ina haki ya kupata asilimia fulani ya maegesho katika eneo lote la Mji Mkongwe, sambamba na kupata asilimia fulani katika bustani ya forodhani.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa mapato yanayotokana na bustani ya Forodhani katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 yalikuwa yanaingizwa katika akaunti ya hesabu ya benki ambayo Mamlaka ilikuwa haitambui, ingawa, wahusika walikuwa baada ya kufanya malipo benki wanawasilisha "statement" Baraza la Manispaa Mjini. Mheshimiwa Spika, kwa mnasaba huo, inaonekana wazi kwamba kuna fedha nyingi ya Serikali inapotea katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasoro hizo zilizobainika na Kamati hii, Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe kuwakodisha nyumba hizo watendaji wake hao. Vile vile, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kukifanyia kazi ipasavyo kifungu cha 42 cha Sheria Namba 4 ya mwaka 2010 ili Mamlaka hii iweze kukusanya mapato yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC ilishtushwa na utaratibu wa Serikali wa kuitaka Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe Zanzibar kuwasilisha baadhi ya mapato yake inayoyakusanya yanayotokana na vibali vya ujenzi na biashara katika Wizara yao na kwa wakati ule ni Wizara ya Ardhi, maji na Nishati. Hivyo, mapato hayo huwa hayaonekani kwenye Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka za Mamlaka, isipokuwa kwamba, hujumuishwa kwenye taarifa za mapato za Wizara na kuonekana kama ni mapato ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo yaliyotolewa na watendaji wa Mamlaka juu ya suala hilo, Kamati ya LAAC iliagiza aliyekuwa Mhasibu wa Wizara hiyo Ndg. Asante Gharib kushiriki katika kikao cha marudio cha kazi za Kamati, ili Kamati iweze kupata taarifa sahihi kutoka kwa mtendaji huyo kwa kuwa katika mwaka huo wa fedha alihusika moja kwa moja na kadhia hiyo.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha mtendaji huyo hakuhudhuria katika kikao hicho muhimu kama alivyotakiwa na Kamati yako kwa madai kwamba yeye hakuondoka na

ofisi, hivyo, wanaowajibika kutoa maelezo ni watendaji waliokuwepo katika Taasisi hiyo kwa wakati ule.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha mtendaji huyo kutohudhuria kwenye kikao hicho halali kimeinyima haki na fursa Kamati yako kupata usahihi wa jambo hilo lililokuwa linatekelezwa kinyume na utaratibu, lakini pia, Kamati yako ilipata mashaka kama kweli fedha hizo zilikuwa zinawasilishwa kama zilivyokusanywa, ingawa, Mamlaka ilikuwa ikitoa stakabadhi ya malipo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati za Baraza zinafanya kazi kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi na kwa kuwa Baraza na Kamati zake zina haki ya kupata taarifa kutoka kwa mtu yeyote, hivyo, kitendo cha mtendaji huyo kutohudhuria kikao hicho ni kuidharau Kamati. Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inaitaka Mamlaka husika ya kinidhamu kumchukulia hatua mtendaji huyo kama Sheria na Kanuni za Utumishi zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuachana na utaratibu wa kuyajumuisha mapato ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe katika kifungu cha mapato cha Wizara na iruhusiwe kuyatolea taarifa mapato yote inayoyakusanya kwa kuwa Mamlaka hii inayo uwezo kisheria wa kutekeleza hilo.

2. Taarifa za Wakaguzi wa Ndani kutofautiana na Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imebaini kuwa takriban asilimia kubwa ya Taasisi tulizozifanyia kazi, Ripoti zao za Mkaguzi wa Hesabu za Ndani zinatofautiana na Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) taarifa ambayo mara nyingi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huifanyia kazi na kutoa mapendekezo yake kwa Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC baada ya kugundua tatizo hilo huwataka Wakaguzi wa Hesabu za Ndani kutoa maelezo yao juu ya taarifa zao na hukiri kuwa taarifa hizo hazipo sahihi kwani mara nyengine huwa wanachukua taarifa kutoka kwenye taarifa za bango kitita taarifa ambazo zilionekana kama hazina uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha taarifa hizo mbili kutoa taarifa tofauti juu ya Taasisi moja kwa jambo moja kinatia dosari utendaji wa Taasisi husika kwani watendaji hao huonekana hawapo makini, lakini pia, inamnyima fursa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kumshauri ipasavyo Mlipaji Mkuu “Paymaster General” wa Serikali kama ilivyoelezwa na kifungu cha 116(2)(h) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, pamoja na kumpotosha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambae pia huwasilishiwa Taarifa hiyo kama ilivyoelezwa na kifungu cha 117(6) cha Sheria hiyo na huitumia Taarifa hiyo wakati wa ukaguzi katika Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inawataka Wakaguzi wa Hesabu za Ndani kuhakikisha kuwa taarifa za fedha wanazipata kutoka katika chanzo cha uhakika ili kupata taarifa sahihi kwani kitendo hicho kitamuwezesha pia Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kutoa ushauri sahihi na wenye tija kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa maslahi ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati ya LAAC inamtaka Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kuwapatia mafunzo Wakaguzi wa Hesabu za Ndani juu ya uandishi wa taarifa (Report) pamoja na kuwaeleza umuhimu wa taarifa wanazoziandaa kwa maendeleo ya nchi na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inashauri hili kwa kuwa baadhi ya taarifa za Wakaguzi wa Hesabu za Ndani zimebainika kuwa na kasoro mbali mbali ikiwemo kukosa taarifa za matumizi wakati kifungu cha 116(2)(h) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, kinamtaka Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kupitia, kutathmini na kupendekeza juu ya mfumo wa usimamizi na ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali. Hivyo, taarifa hizo zikiwa na kasoro zitampelekea Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kutoa mapendekezo yaliyokuwa hayana uhalisia na ataipotosha Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 117(1)(6) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Wakaguzi wa Hesabu za Ndani wanatakiwa moja kwa moja kuwasilisha taarifa zao za robo mwaka na za mwaka kwa Mkuu wa Hazina “Tresury” ambaye baada ya kupokea taarifa hizo kwa mujibu wa utaratibu wao wa ndani huziwasilisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kwa ajili ya kuzifanyia kazi kama Sheria inavyomuelekeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, Kamati ya LAAC imegundua hakuna uhusiano wa karibu “closely relationship” baina ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani na Wakaguzi wa Hesabu za Ndani. Hivyo, ili kuwa na uhusiano wa karibu baina ya watu wawili hawa na hasa ukizingatia majukumu makubwa aliyopewa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani na Sheria hiyo pamoja na kuondosha urasimu wa kiutendaji, Kamati hii inaiomba Serikali kukifanyia marekebisho kifungu hicho na kuweka masharti yatakayowawezesha Wakaguzi wa Hesabu za Ndani kuwasilisha moja kwa moja taarifa zao kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani na baadae Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani ndio awasilishe taarifa hizo kwa Mkuu wa Hazina.

3. Kuundwa kwa Kamati za Ukaguzi wa Ndani

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kw Mashirika na Taasisi Zinazojitegema za Serikali ya mwaka wa fedha 2019/2020 ilibaini kuwa baadhi ya Taasisi hizo kupitia Afisa Mhasibu hazikuunda Kamati ya Ukaguzi wa Ndani jambo ambalo ni kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka

2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaunga mkono hoja ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kutokuwepo Kamati hizo katika Taasisi azilozibainisha, isipokuwa kwamba, Kamati hiyo inapaswa kuundwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi husika badala ya Afisa Mhasibu kama alivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi Zinazojitegemea kufuata masharti yaliyoelezwa na kifungu cha 118(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni ya 148(4) ya Kanuni za Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya Taasisi hizo hutumia kifungu kilichomo ndani ya Sheria ya Taasisi husika kinachoipa mamlaka Bodi kuunda Kamati. Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inazieleza Taasisi hizo kuwa, Kamati zilizoelezwa kwenye Sheria zao ni zile Kamati nyengine za kuisaidia Bodi kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia Taasisi husika kwa mfano Kamati za Fedha na Utawala na sio Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ambayo inaundwa kwa mujibu wa kifungu cha 118(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Taasisi ambazo zinatumia kifungu kilichomo kwenye Sheria yake kuunda Kamati hiyo ni Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ambayo hutumia kifungu cha 17(f) cha Sheria hiyo, Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) ambayo hutumia kifungu namba 12 kilichoanishwa katika Jadweli nambari moja (1) ya Sheria ya Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasoro hiyo iliyobainika, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi zote zenye uasili kama huo kuacha kufuata utaratibu huo na kuunda Kamati hizo mara moja kama ilivyoelezwa na kifungu cha 118(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati ya LAAC inawashauri watendaji wa Serikali kuachana na tabia ya kufanya kazi kwa mazowea na kuitumia Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa kisheria kwa kuwa Afisi hiyo pamoja na mambo mengine ina jukumu hilo kwa mujibu wa kifungu cha 56 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na sio kufanya kazi kama wanavyoona wao inafaa kwa lengo la kuepusha hoja zisizo na msingi.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani na zilizoundwa pasi na kuzingatia sheria inapelekea kukosa maoni na ushauri juu ya taarifa zinazotolewa na Mkaguzi wa Hesabu za Ndani na Mkaguzi wa Nje.

4. **Baadhi ya Maagizo ya Serikali kuzikwaza Taasisi za Umma**

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya maagizo yanayotolewa na Serikali huzikwaza Taasisi zake kwa kuwa tayari Taasisi hizo zina mipango na malengo yao ya kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii inaunga mkono hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya uanzishwaji wa Kampuni ya ZAFICO na kuziona Taasisi hizo kuwa zimeingia kwenye uwekezaji usio na tija na hatimae kuonekana kutumika vibaya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia hoja hii, takriban Taasisi nyingi ambazo nyengine ni Wanahisa (Shareholders) zilikiri kuwepo kwa upungufu katika utekelezaji wa Kampuni hiyo, jambo ambalo limepelekea baadhi ya Taasisi kuwa na kigugumizi cha kutoa fedha zake baada ya kuona kuwa uwekezaji huo hauna tija. Mheshimiwa Spika, hadi Kamati hii inafanya kazi zake katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) umewekeza jumla ya Tsh. bilioni 3.15 na hakuna tija yoyote iliyopatikana.

Mheshimiwa Spika, mfano wa agizo jengine lililotolewa na Serikali ambalo limeonekana halina tija ni kuzitaka Taasisi zake kufunga hesabu za mwisho wa mwaka kwa kutumia mfumo wa "Cash Basis", jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Mashirika kwa mujibu wa viwango vya kihasibu (Financial Accounting Standards) vilivyopo kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, endapo Taasisi itatumia mfumo huo baadhi ya taarifa muhimu hazitoonekana, taarifa ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa Shirika husika kifaida au hasara pamoja na kutojulikana kwa madeni yanayodaiwa na yanayodai Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mfumo huo una mapungufu yake, Kamati ya LAAC inaitaka Serikali kuziruhusu Taasisi zake kufunga hesabu za mwisho wa mwaka kwa kutumia Mfumo wa "Accrual Basis", mfumo ambao unajumuisha taarifa zote zikiwemo za uchakavu wa mali na uwezo sahihi wa kifedha wa Taasisi ambao hutoa taarifa halisi na sahihi.

5. Kuwepo kwa sehemu ya taarifa ya fedha "Segment Report" kwa Taasisi zilizopo Pemba

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC ilishindwa kupima utendaji wa Taasisi za Pemba kwa kuwa taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo hujumuishwa moja kwa moja kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ya Makao Makuu ya Taasisi hiyo yaliopo Unguja kwa kuwa Taasisi za Pemba ni sehemu tu ya Taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo hili lilipelekea Kamati ya LAAC kupokea taarifa mbili tofauti kwa baadhi ya Taasisi hizo (yaani Makao Makuu ina taarifa yake ya mapato na Pemba

wana taarifa nyengine). Hivyo, kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuanzisha mfumo wa kuwa na “segment report” kwa lengo la kupata taarifa sahihi za Pemba kwa kuwa mfumo huo unakubalika kimataifa.

6. Kuwepo mgongano wa Sheria

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC katika kutekeleza majukumu yake ilipokea malalamiko kadhaa juu ya ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2019/2020 uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Baadhi ya malalamiko hayo ni pamoja na Taasisi kutokupatiwa muda wa kutosha wa kujibu hoja zilizojitokeza katika Taasisi hizo ambapo kwa mujibu wa kifungu cha 47(8) cha Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali namba 11 ya mwaka 2003 Taasisi husika inatakiwa ijibu hoja hizo sio zaidi ya siku 30. Vile vile, baadhi ya barua kutoka Afisi ya Mdhibiti zinazozitaka Taasisi kujibu hoja zilizojitokeza kwenye Taasisi husika zilichelewa kuwafika walengwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC ilitaka kujiridhisha na kile kinacholalamikiwa na ilimtaka Afisa wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anayefuatana na Kamati kutoa maelezo juu ya tuhuma hizo hususan kwa upande wa Taasisi kupatiwa muda mchache kinyume na ilivyozoweleka. Mtendaji huyo aliieleza Kamati kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 123(4) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa ndani ya miezi saba baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha kuandaa ripoti ya ukaguzi na kuiwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi. Hivyo, katika mwaka huo wa fedha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alitumia kifungu hicho cha Sheria.

Mheshimiwa Spika, Mtendaji huyo alizidi kuieleza Kamati hii kuwa, kwa kuwa muda wa utayarishaji wa taarifa za fedha za mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma haukubadilika, na kwa kuwa mwaka huo uliambatana na Uchaguzi Mkuu wa Kitaifa, zoezi la ukaguzi lilichukua muda kutokana na changamoto za upatikanaji wa taarifa za fedha pamoja na Watendaji Wakuu wa Taasisi zinazokaguliwa. Hali hiyo ilipelekea Wakaguzi kupunguza muda wa kupokea majibu na kufikia wiki mbili wakiamini muda huo unatosha kuwasilisha majibu ya hoja ili kuweza kukamilisha taratibu za uwasilishaji wa Ripoti ya Mdhibiti kwa Mheshimiwa Rais pamoja na Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuzifanyia marekebisho Sheria hizo ili ziwe na kauli moja kiutendaji kwa dhamira ya kuimarisha misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inashauri hili kwa kuwa kifungu cha 58(1) cha Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

za Serikali kuandaa ripoti ya ukaguzi ndani ya siku tisini baada ya mwisho wa mwaka wa fedha na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais, ambaye kwa mujibu wa kifungu cha 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Baraza la Wawakilishi kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo.

7. Baadhi ya Taasisi za Umma kuruhusiwa na Serikali kukodisha majengo yao na Taasisi nyengine kunyimwa fursa hiyo

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imebaini kuwa jumla ya Wizara tatu ambazo ni: Wizara ya Uchumi wa Bluu, Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi, na Taasisi mbili za Serikali ambazo ni Kampuni ya Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Zanzibar (ZPDC) na Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) zinatumia jengo la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) bila ya kulipa kodi wakati baadhi ya Taasisi za Serikali hutumia majengo ya Taasisi nyengine kwa kukodi.

Mheshimiwa Spika, mfano wa Taasisi ya Serikali ambayo inakodisha jengo lake kwa Taasisi nyengine ya Serikali ni Mfuko wa Barabara ambapo Mamlaka hii pia kabla ya kujenga jengo lake ilikodi ofisi katika jengo hilo na hivi sasa Mfuko wa Barabara umeikodisha ofisi ya Mkaguzi Kuu wa Hesabu za Ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023 kuiruhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) kuzikodisha Taasisi zote zinazotumia jengo hilo, ili Mamlaka nayo iweze kukusanya mapato kupitia jengo lake kwa nia ya kuimarisha utendaji wa Mamlaka, kuepusha usumbufu wa malipo katika huduma zinazotolewa, kuendeleza muonekano mzuri wa jengo na haiba yake (Maintanance and services) pamoja na kuiongezea mapato Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inashauri hilo kwa kuwa endapo Mamlaka hii itakodisha jengo lake kwa kukisia itakusanya takriban jumla ya Tsh. 70,560,000 kwa mwezi sawa na Tsh. 846,720,000 kwa mwaka au USD 29,400 kwa mwezi sawa na USD 352,800 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imebaini kuwa Wizara na Taasisi zinazotumia jengo hilo hazilipi ipasavyo huduma inazotumia kama vile ulinzi, umeme, kodi ya ardhi, mafuta ya jenereta, usafi na maji. Kitendo hicho kinakigharimu sana Mamlaka hii kutumia fedha nyingi kwa mambo ambayo hayahusu Mamlaka moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati hulazimika

kulipia gharama hizo kwa kuwa ndio mmiliki wa jengo hilo na gharama hizo huwasilishwa moja kwa moja kwake na Taasisi husika (yaani wenye kutoa huduma).

Mheshimiwa Spika, katika kuthibitisha hili, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati kwa mfano kuanzia mwezi wa Oktoba hadi Disemba, 2021 imetumia jumla Tsh. 74,975,810 kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa jengo matumizi ambayo yamevuka makisio ya bajeti husika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, gharama za madeni huzidi kila mwezi kutokana na kutokulipwa kwa huduma zinazotumika kwa muda uliopangwa. Mheshimiwa Spika, ukiacha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati, Taasisi zinazotumia jengo hilo hadi Disemba, 2021 zinadaiwa baadhi ya gharama zifuatazo:

1. Wizara ya Maji, Nishati na Madini inadaiwa Tsh. 3,387,989 ikiwa ni 10% ya matengenezo ya Lifti na Air Condition;

2. Umeme Tsh. 68,849,849;

3. Mafuta ya jenereta hadi tarehe 31 Januari, 2022 Taasisi hizo zinadaiwa kama ifuatavyo:
   a. Kampuni ya Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Zanzibar (ZPDC) asilimia 15 sawa na Tsh. 416,700;

   b. Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asili (ZPRA) asilimia 15 sawa na Tsh. 416,700;

   c. Wizara ya Maji, Nishati na Madini 10% sawa na Tsh. 277,800;

   d. Wizara ya Ardhi, na Maendeleo ya Makazi 10% sawa na Tsh. 277,800; na

   e. Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi 10% sawa na Tsh. 277,800

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inazitaka Wizara na Taasisi zote zilizopo katika jengo hilo kulipia gharama mbali mbali zinazotumia ili kuiondoshea Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati mzigo uliokuwa hauna msingi.

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali kuziruhusu Wizara na Taasisi zake kutumia jengo la

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati bure bado Mamlaka hii inatakiwa kulipa kodi ya ardhi (Lease) kwa Serikali jumla ya USD 1000 kila mwaka wakati Wizara inayohusika na masuala ya ardhi pia inatumia eneo au jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati inatozwa kodi ya ardhi, na kwa kuwa Wizara na Taasisi za Serikali zinazotumia jengo hilo zinakaa bure, hivyo basi, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kutoilipisha Mamlaka hiyo kodi ya ardhi hadi hapo Wizara na Taasisi zinazotumia jengo hilo zitaanza kulipa kodi ya pango.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Kamati ya LAAC haikuridhika na namna Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati inavyotumia gharama kubwa kwa ajili ya kulisimamia na kuliendeleza jengo lake kwa maslahi ya Taasisi nyengine, Taasisi ambazo pia huingiziwa fedha kwa matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuyatekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Kamati hii kwa maslahi ya utendaji mzuri wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati.

8. **Baadhi ya Watendaji wa Serikali kutekeleza mambo kinyume na maagizo ya Mheshimiwa Rais**

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC wakati inafuatilia hoja namba **3.1.1** kuhusiana na *"Mapungufu katika daftari la kuhifadhia Mali za kudumu"* iliyoripotiwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), na wakati Kamati hii inafuatilia matumizi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilibaini kuwa baadhi ya watendaji wa Serikali hutekeleza mambo kinyume na maagizo yanayotolewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC ilidiriki kusema hivyo baada ya watendaji wa Ofisi ya Rais – Ikulu kutekeleza agizo lililotolewa na Mheshimiwa Rais kupitia barua ya tarehe 10 Februari, 2021 iliyowekwa saini na Kaimu Katibu wa Rais kulitekeleza agizo hilo kinyume na matakwa na mantiki ya agizo husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa agizo la kuchukuliwa gari za Serikali zilizokuwa zikitumiwa na Naibu Mawaziri, Naibu Makatibu Wakuu na gari zote zilizotelekezwa kwenye maegesho na magereji.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyojitokeza katika utekelezaji wa agizo hilo ni kwamba, Watendaji hao walichukua hata gari zilizokuwa zinatumika kama kawaida na Taasisi hizo, gazi ambayo tayari imeshauzwa kwa mtu na gari ambazo zilikuwa zinasubiria vifaa kwa ajili ya matengenezo, ambapo jumla ya gari 18 za Shirika la

Umeme zilichukuliwa na kwa upande wa Mamlaka ya Maji jumla ya gari 14 zilichukuliwa. Gari zote hizo zilihifadhiwa katika kiwanja cha Mamlaka ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA).

Mheshimiwa Spika, mfano wa gari za Shirika la Umeme zilizochukuliwa ambazo zilikuwa zinatumika ni Prado - SLS 159A lililokuwa linatumiwa na Mkurugenzi Fedha na Mipango na Suzuki Escudo - SLS 176A iliyokuwa inatumiwa na Afisi ya Mhasibu na kwa upande wa gari zilizokuwa kwenye matengenezo ni Toyota Town Ace - SLS 198B gari iliyokuwa inatumika Wilaya ya Kaskazini “A” gari ambayo ilibebwa ikiwa na Fundi kwenye matengenezo na gari aina ya Toyota Land Cruiser - SMZ 5362 iliyokuwa inatumiwa na Idara ya Ufundi, kwa kazi za Ufundi - Mtandao wa Maji.

Mheshimiwa Spika, gari nyengine zilizochukuliwa ni gari ambazo zilizokuwa hazijatengenezwa, isipokuwa kwamba, gari hizo zinasubiri vifaa. Gari zenyewe ni Toyota Town Ace - SLS 190B iliyokuwa inatumika Wilaya ya Kaskazini “B” kwa kazi za Operesheni za Wilaya, Toyota Town Ace - SLS 202B iliyokuwa inatumika Wilaya ya Kusini kwa kazi za Operesheni za Wilaya, Toyota Hilux - SLS 225B iliyokuwa inatumika Wilaya Kaskazini “B” kwa ajili ya Operesheni za Wilaya, Nissan Hard Bod - SLS 151B iliyokuwa inatukiwa na Afisi Kuu - Idara ya Rasilimali Maji, Suzuki Vitara - SLS 158A.

Mheshimiwa Spika, kuchukuliwa kwa gari hizo kwa kiasi kikubwa kumerudisha nyuma utendaji wa Taasisi hizi na kumepelekea baadhi ya Watendaji ambao wana haki ya kuwa na usafiri kukosa haki yao hiyo ya msingi. Kwa mantiki hiyo, kitendo cha kuchukua gari zilizokuwa zinatumika hakikuwa halali kwa mujibu wa utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC haipingani na agizo lililotolewa na Mheshimiwa Rais, isipokuwa kwamba, inapinga utaratibu uliotumiwa na watendaji wa Ofisi yake ya kuchukua gari hizo bila ya kujuulishwa Mkuu wa Taasisi na kwa Taasisi nyengine Mkuu wa Taasisi alipata taarifa ya kuchukuliwa gari hizo baada ya Mkuu wa Magari ya Taasisi husika kuzuwia uchukuaji huo usiofuata taratibu.

Mheshimiwa Spika, kitendo hicho kilizua mtaharuki baina ya watendaji wa Serikali na hata kupelekea baadhi ya Taasisi kwa mfano Mamlaka ya Maji kuilalamikia na kuomba muongozo kwa Wizara yake juu ya zoezi hilo na kuarifiwa kuwa waridhie kuchukuliwa kwa gari hizo pasi na kumpatia nakala ya barua husika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kamati ya LAAC ililazimika kuandaa kikao cha pamoja na Watendaji wa ZAWA, ZECO, Katibu Mkuu – Afisi ya Rais Ikulu na Mkuu wa Magari wa Afisi ya Rais Ikulu tarehe 02 Februari, 2022 ili kujua kiini ya kile kilichokuwa kinalalamikiwa hasa ikizingatiwa kuwa kwa kawaida msema pweke huwa hana makosa.

Mheshimiwa Spika, ingawa watendaji wa Ikulu waliieleza Kamati kuwa agizo hilo lilitekelezwa kwa njia ya kushtukiza ili Taasisi husika zisipate muda wa kuzificha gari hizo, hata hivyo, watendaji wa Ikulu walipaswa siku ya tukio kufika ofisini kwa Mkuu wa Taasisi na kumuonesha agizo hilo kwa kuwa Mkuu huyo ndio mas'uul kwa gari hizo.

Mheshimiwa Spika, Watendaji wa Ikulu katika kuhalalisha utaratibu walioutumia wa kuchukua gari hizo na kuonekana kama Mamlaka ya Maji na Shirika la Umeme wamefanya uzembe juu ya zoezi hilo, waliieleza Kamati kuwa baada ya zoezi la uchukuaji gari kukamilika kila Taasisi iliyochukuliwa gari zake ilitakiwa kuzichukua gari hizo na kuzifanyia matengenezo kwa lengo la kutumika na kwa zile gari ambazo hawawezi kuzitengeneza basi ichukuliwe hatua ya kuuzwa na Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, hata hivyo, baadhi ya Taasisi hazikufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, Kamati ya LAAC iliwauliza Watendaji wa ZECO na ZAWA mbele ya Watendaji wa Ikulu juu ya jambo hilo, ambao kwa pamoja hawakukubaliana na kauli hiyo na walizidi kusisitiza kuwa hawakupokea taarifa yoyote kuhusiana na maelekezo hayo. Isipokuwa kwamba, Shirika la Umeme lilipokea barua kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kutakiwa kuwasilisha kadi na funguo za baadhi ya gari zilizochukuliwa barua ya tarehe 23 Septemba, 2021 yenye kumbukumbu Namba BA.26/454/01/21/12 inahusika na kwa upande wa Mamlaka ya Maji barua ya tarehe 12 Oktoba, 2021 yenye kumbukumbu namba ZAWA/A 10/3/VOL.IV/31 inahusika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa taarifa zinazotolewa mbele ya Kamati zinatakiwa kuwa ni taarifa sahihi, hivyo basi, Kamati hii iliomba kupatiwa barua iliyotoa maelekezo au muongozo huo ili kujiridhisha na kile kilichoelezwa na Watendaji hao. Hata hivyo, Watendaji wa Ikulu waliieleza Kamati kuwa barua hiyo haipo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kauli hiyo, Kamati ya LAAC ilizidi kupata mashaka juu ya usahihi wa taarifa zilizokuwa zinatolewa na Watendaji wa Ikulu hasa ikizingatiwa kuwa kwa mujibu wa kanuni ya 48(2) ya Kanuni ya Utumishi ya mwaka 2014, mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali yanatakiwa kuwa kwa maandishi jambo ambalo inaonekana kuwa halikufanyika.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuuza mali za Taasisi hizo bila ya kuzishirikisha Taasisi husika ni kwenda kinyume na kifungu cha 43(3) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji Mali za Umma ya mwaka 2016. Kwani kifungu hiki kinaeleza kuwa uondoaji wa mali lazima uidhinishwe na Afisa Mhasibu (yaani Mtendaji Mkuu wa Taasisi) kabla ya kuanza hatua ya uondoshaji wa mali husika, isipokuwa kwamba, katika kadhia hii Watendaji hao walitakiwa kuwasilisha funguo na kadi za gari tu.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, Kamati ya LAAC inalieleza Baraza lako

kuwa gari zote za ZAWA zilizochukuliwa na kupelekwa katika kiwanja cha ZAECA hazipo tena katika kiwanja hicho na wala hakuna mawasiliano yoyote juu ya kadhia hiyo na Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watendaji wa Ikulu walitekeleza agizo la Mheshimiwa Rais kinyume na alivyoelekeza, na kwa kuwa miongoni mwa mambo yaliyokiukwa ni kuvunjwa kwa kanuni ya 48(2) ya Kanuni za Utumishi ya mwaka 2014. Hivyo basi, Kamati ya LAAC haina budi kutamka kuwa haikuridhika na utaratibu uliotumika juu ya utekelezwaji wa agizo hilo halali la Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inapendekeza yafuatayo:

1. Gari zilizochukuliwa na kufanyiwa matengenezo zirejeshwe kwa Taasisi husika kutokana na tatizo la uhaba wa gari katika Taasisi hizo na endapo Serikali itazihitaji gari hizo basi utaratibu wa kisheria ufuatwe.

2. Endapo kuna gharama zozote zilitumika kwa kuzifanyia matengenezo gari hizo basi Taasisi husika ipatiwe stakabadhi za malipo yaliyofanywa ili iweze kufanya marejesho kwa Taasisi iliyotengeneza.

3. Watendaji wa Serikali, wahakikishe kuwa wanatekeleza shughuli zao kama Sheria, Kanuni na taratibu za nchi zinavyoelekeza badala ya kufuata utashi wao ili kulinda nidhamu ya utendaji na uwajibikaji.

4. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afuatilie kwa kina namna zoezi hilo lilivyotekelezwa pamoja na kujua gari hizo 32 zimeishia katika mikono ya nani, ili kujiridhisha kuwa baadhi ya gari hizo hazikuishia mikononi mwa watu visivyo halali.

9. Bodi za Wakurugenzi kuridhia makosa yanayofanywa na Watendaji

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC katika kutekeleza majukumu yake ilibaini kuwa baadhi ya Bodi za Wakurugenzi huridhia makosa yanayofanywa na Watendaji jambo linalopelekea watendaji hao kuzidharau Bodi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC ilibaini kasoro hiyo, ilivyofanya uchunguzi Shirika la Magazeti la Zanzibar ambapo ilibaini kuwa Mhariri Mtendaji alikuwa Mjumbe wa Bodi kwa mujibu wa kifungu cha 11(e) cha Sheria ya Magazeti namba 11 ya mwaka 2008 lakini pia, Bodi ilimteua kuwa ni Katibu wa Bodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ingawa kifungu cha 11(3) cha Sheria hiyo hakikueleza Katibu wa

Bodi atateuliwa kutoka wapi, hata hivyo, uzoefu unaonesha kuwa Mjumbe wa Bodi hawezi kuwa Katibu wa Bodi hiyo pia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzito na wingi wa majukumu ya Mhariri Mtendaji kazi za Ukatibu zilikuwa hazitekelezi ipasavyo na jambo la kushangaza Bodi hiyo ilimridhia kutekeleza shughuli hizo pamoja na upungufu wake.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia baadhi ya mambo yaliyoamuliwa na Bodi, Kamati yako iliomba kupatiwa kumbukumbu za kikao husika, hata hivyo, kumbukumbu hizo zilieleza tu kuwa jambo fulani lilikuwa ni miongoni mwa ajenda ya kikao husika, na hakukuwa na maelezo ya kina juu ya maamuzi ya ajenda hiyo kitendo ambacho ni kinyume na uandishi wa kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Katibu huyo alikuwa hahifadhi vyema nyaraka na kumbukumbu za vikao jambo lililopelekea kukosekana kwa nyaraka na kumbukumbu nyingi za vikao hivyo. Kitendo hicho, inamnyima mtu kufanya rejea juu ya maamuzi ya Bodi kwa jambo lililoamuliwa katika miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, Licha ya kasoro hiyo iliyoelezwa na Kamati hii, kwa ujumla Kamati ya LAAC haikuridhishwa na utendaji kazi wa Uongozi wa Shirika la Magazeti chini ya Mhariri Mtendaji Ndg. Yussuf Khamis.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imediriki kutamka hivyo kutokana na kuwa ilipofika katika Shirika hilo kufuatilia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya mwaka wa fedha 2017/2018 ilishindwa kufanya shughuli hiyo kwa ufanisi kwa madai kwamba Mhasibu wa Shirika alikuwa likizo ya uzazi na hakukuwa na mtu mwengine wa kujibu hoja za Kamati, licha ya kuwa taarifa ya kufanya kazi hiyo ilifika ofisini hapo siku nyingi kabla ya kikao hicho.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC ililazimika kuahirisha kikao hicho baada ya kuona kwamba Uongozi wa Shirika haukulipa uzito suala hilo na hata wakati wa majadiliano Uongozi huo haukuonesha kama unajutia kwa kile ambacho kimetokezea na Kamati yako iliamini kuwa imedharauliwa kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati za Baraza zinafanya kazi kwa niaba ya Baraza na kwa kuwa Baraza na Kamati zake zina haki ya kupata taarifa kutoka kwa Serikali ili liweze kuisimamia Serikali ipasavyo na kutoa ushauri wenye tija kwa maslahi ya nchi na kwa taifa kwa ujumla. Hivyo basi, Kamati ya LAAC inaitaka Serikali kumchukulia hatua za kinidhamu aliyekuwa Mhariri Mtendaji ili iwe funzo kwa watendaji wengine wenye

malengo hasi kama yeye.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imelazimika kushauri hivyo kwa kuwa Kamati hiyo ilivyofanya ziara yake ya kufuatilia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliagiza kuwa wahudhurie kwenye kikao wale wote waliohusika na kadhia ya mwaka huo ili Kamati iweze kupata majibu sahihi. Hata hivyo, Mtendaji huyo hakuhudhuria kwenye kikao hicho bila ya kutoa dharura yoyote kwa Mwenyekiti wa Kamati, ingawa Mwenyekiti wa Bodi pamoja na Mhariri Mtendaji wa hivi sasa kumjulisha jambo hilo.

10. Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kutojibu barua za Taasisi nyengine kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, takriban asilimia kubwa ya Taasisi za Serikali zimetoa malalamiko kwa Kamati hii kuhusiana na tatizo la Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kutojibu barua za Taasisi nyengine kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni kasoro kubwa ya kiutendaji na hata hupelekea baadhi ya Taasisi kupata hoja ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutokana na kukosekana kwa barua kutoka katika Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mfano wa Taasisi ambayo ilipata hoja ya Mkaguzi Mkuu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kutokana na kasoro hiyo ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ambayo ilipata hoja nambari 3.8.5 kuhusiana na *"Kukosekana kwa uthibitisho kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa malipo ya gharama za awali za Mradi wa Mji Mpya Kwahani Tsh. Bilioni 1.19"* (kwa maelezo zaidi tafadhali rejea ukurasa wa 93 wa Ripoti ya Mdhibiti).

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC ililisimamia suala hilo ipasavyo kwa kuwaita Watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa lengo la kujua changamoto inayowakabili hata wakachelewa kutoa barua hiyo, ambapo, Kamati hii ilibaini kuwa hakukuwa na sababu ya msingi ya kuchelewa kujibu barua hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC iliwataka Watendaji wa Ofisi hiyo kuijibu barua hiyo ndani ya siku tatu na nakala ya barua hiyo apatiwe Mwenyekiti

wa Kamati ili ajiridhishe kama agizo hilo limetekelzwa ipasavyo kwa dhamira ya kufutwa hoja hiyo na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa bashasha kubwa, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa barua hiyo tayari imeshajibiwa kama Kamati ilivyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inasikitishwa na kitendo cha Ofisi hiyo na hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya Taasisi hupeleka barua katika Ofisi hiyo kwa lengo la kupata muongozo juu ya jambo husika kwa maslahi ya nchi, hata hivyo, jambo hilo hukwama kutekelezwa kutokana na dharau za watendaji wa Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mfano wa Taasisi ambayo imeomba muongozo na haikujibiwa hadi Kamati yako inafanya ziara katika Taasisi hiyo tarehe 01 Februari, 2022 ni Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA).

Mheshimiwa Spika, Mamlaka hiyo iliiandikia barua Afisi hiyo tangu tarehe 22 Julai, 2021 barua yenye kumbukumbu Namba ZMA/(OR) FNM/255/4/VOL. II, kwa lengo la kuomba muongozo na ruhusa ya utoaji wa risiti kwa njia ya kielektroniki na tayari mashine za shughuli hiyo zimeshanunuliwa.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha watendaji wa Afisi hiyo kutokutoa muongozo kwa kitu kama hiki muhimu ni kurudisha nyuma juhudi za Serikali hii, kwani Serikali inasisitiza malipo ya Taasisi kufanywa kwa kutumia mashine za kielektroniki na sio kutumia vitabu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inamtaka Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuliondoa tatizo hilo mara moja kwenye Taasisi yake, hasa ikizingatiwa kuwa Ofisi hiyo ndio tegemeo la nchi.

11. Asilimia kubwa ya Taasisi za Serikali hazilipi huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Maji na Shirika la Umeme

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imesikitishwa sana na kitendo cha Taasisi za Serikali kutolipa huduma ya umeme na maji wakati Baraza la Wawakilishi huidhinisha fedha kwa ajili ya matumizi ya shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Taasisi hazilipi fedha za huduma hizo na hupelekea baada ya kipindi fulani Serikali kulipa fedha hizo kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina ama kuyasamehe madeni yaliyopo. Hivyo basi, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuanzia mwezi wa Machi, 2022 kuzikata Taasisi zake fedha za huduma hizo moja kwa moja kwenye fedha zao za Matumizi Mengineyo (OC) ili kuepusha kasoro hiyo.

12. Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka kinyume na taratibu za Kitaifa na

Kimataifa

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imebaini kuwa asilimia kubwa ya Wahasibu hufunga hesabu za mwisho wa mwaka kinyume na utaratibu, ingawa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huzifanyia marekebisho taarifa hizo lakini bado zinakuwa na makosa makubwa.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mapungufu yaliyobainika na Kamati ni pamoja na:

1. Ufafanuzi wa kihasibu (Note) moja kuwa na zaidi ya matumizi ya aina moja;

2. Kuandikwa kuwa bajeti husika imefanyiwa mapitio wakati uhalisia haupo hivyo;

3. Baadhi ya "Note" hazina ufafanuzi;

4. "Note" moja kuwa na zaidi ya kiwango kimoja cha fedha, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuwapatia mafunzo Wahasibu wake wote ili kuwa na ufahamu wa pamoja juu ya uandishi wa Taarifa hiyo.

13. Taasisi Zinazojitegemea za Serikali hutakiwa na baadhi ya Wizara zao kuzihudumia

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imebaini kwa baadhi ya Wizara huzilazimisha Taasisi Zinazojitegemea za Serikali zilizopo ndani ya Wizara hizo kuzihudumia Wizara zao jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, tatizo hilo limebainika kwa kiasi kikubwa katika iliyokuwa Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati wakati Kamati hii ilivyokuwa inafuatilia Ripoti ya Mdhibiti ya mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo, Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) ilionekana kufanya matumizi kwa ajili ya Wizara. Kwa mfano, kugharamia mafuta ya gari ya Mheshimiwa Waziri, kusaidia gharama za safari za Mheshimiwa Waziri au Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kila Wizara huidhinishiwa bajeti ya matumizi na Baraza hili ni vyema kila Wizara ikafanya matumizi kwa mujibu wa bajeti yake na sio kuzikwaza Taasisi nyengine.

14. Kamati ya LAAC kushindwa kutekeleza vyema majukumu yake kwa baadhi ya Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC ilishindwa kutekeleza vyema majukumu yake kwa baadhi ya Serikali za Mitaa kutokana na asilimia kubwa ya Watendaji wa Mabaraza na Halmashauri hizo kuwa wapya jambo lililopelekea Watendaji hao kushindwa kujibu kwa ufasaha hoja za Wajumbe.

Mheshimiwa Spika, licha ya Kamati yako kuagiza kuwepo Watendaji wote waliohusika na mwaka wa fedha husika, hata hivyo, Watendaji hao hawakuhudhuria na kwa yale Mabaraza ambayo Watendaji hao walihudhuria basi walishindwa kujibu hoja za Kamati kwa madai kwamba siku nyingi zimepita hivyo hawakumbuki tena kilichotokea. Miongoni mwa Mabaraza ambayo Kamati hii haikufanya kazi ipasavyo ni Baraza la Mji Mkoani, Baraza la Mji Chake Chake na Baraza la Mji Wete.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, kwa ujumla Kamati ya LAAC imehisi bado kuna kazi kubwa kwa Serikali Kuu katika kuzisimamia Serikali za Mitaa kwani asilimia kubwa ya Watendaji wa Taasisi hizo hawajabobea katika kazi zao na baadhi ya maeneo hayana Watendaji wenye sifa zinazostahiki hususan kwenye eneo la ukusanyaji wa mapato. Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali Kuu kuzidi kuwa karibu na Taasisi hizo pamoja na kuzifanyia marekebisho makubwa Taasisi hizo.

15. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo naomba nimalizie muhtasari huu kwa kuziomba Taasisi za Serikali kuipa mashirikiano ya dhati Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale inapotekeleza jukumu lake pamoja na kufanya mapema maandalizi juu ya mwaka husika unaokaguliwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imelazimika kulisema hili kwa kuwa baadhi ya hoja huandikwa na Mkaguzi Mkuu baada ya kukosa maelezo kwa wahusika, isipokuwa kwamba, inapokwenda Kamati hupata maelezo ya kina na endapo Kamati itawauliza Watendaji kwa nini majibu kama hayo wasimpatie Mkaguzi basi Watendaji hao huwa hawana majibu. Hivyo, ni busara kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Taasisi zinazokaguliwa kukabidhiana kumbukumbu za ukaguzi kwa maandishi ili kuwa na uthibitisho wa zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuiongezea fedha za matumizi Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwa lengo la kuzijengea uwezo Kamati ya LAAC na Kamati ya PAC kama zinavyofanya nchi nyengine duniani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC inashauri hili kwa kuwa Ofisi hiyo ilikaribia kushindwa kuwapatia uchambuzi wa Ripoti zake za mwaka wa fedha 2019/2020 Wajumbe wa Kamati hizo kutokana na uhaba wa fedha unaoukabili Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, licha ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kuruhusiwa kukodi (hire) mtu yoyote katika kutekeleza shughuli zake, hata hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Ofisi hiyo kuajiri Watendaji wenye sifa, taaluma na fani tofauti ili Ofisi yake iweze kutekeleza shughuli zake bila ya usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya LAAC imelazimika kulishauri hili kwa kuwa unapomkodi mtu inakugharimu kiasi kikubwa cha fedha tofauti na kumuajiri mtu huyo.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Kamati hii kuwa Serikali itazifanyia kazi kasoro zote zilizozibainika na Kamati pamoja na kuyatekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza na ninawaomba waijadili na hatimae kuipitisha Ripoti ya Kamati ya LAAC kwa lengo la kutekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

…………………

Habib Ali Mohammed,
Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.